



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA MAJITAKA DAR ES SALAAM

TAARIFA KWA UMMA

DAWASA: MAMLAKA PEKEE YA MAJI ILIYOTOA GAWIO LA BN 3.45 SERIKALINI

Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) ni moja ya Taasisi za umma ambazo leo zimekabidhi rasmi hundi za michango yao kwa Serikali, kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dk. John Pombe Magufuli.

Katika hafla hiyo iliyofanyika katika ukumbi wa kimataifa wa mikutano wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es salaam, Mwenyekiti wa Bodi ya DAWASA Jenerali mstafu Davis Mwamunyange alimkabidhi Mheshimiwa Rais hundi ya mfano ya kiasi cha **shilingi 3,450,121,580.15**, ikiwa ni gawio lililotolewa katika mwaka wa fedha 2016/17. DAWASA ndiyo Mamlaka pekee ya Maji nchini ambayo imeweza kutoa gawio serikalini.

DAWASA ilijumishwa rasmi kwenye orodha ya taasisi za umma zinazotakiwa kuchangia asilimia 15 ya mapato yake ghafi kwenye Mfuko Mkuu Wa Hazina mwaka 2016 na ilianza kuchangia mwezi Julai 2016.

Tangu kipindi hicho, DAWASA imekuwa ikichangia asilimia 15 ya mapato yake ghafi (gross revenue collection) kila mwezi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Katika mwaka 2016/17 ilichangia kiasi cha **shilingi bilioni 3.48** na kiasi cha **shilingi bilioni 3.45** kimewasilishwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18.

Aidha katika mwaka mpya wa fedha 2018/19, tayari DAWASA imeshalipa kiasi cha **shilingi milioni 482** kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ambayo ni asilimia 15 ya mapato ghafi kwa kipindi cha mwezi Mei na mwezi Juni 2018 na imelipa kiasi cha **shilingi milioni 500** kama gawio kutokana na ziada iliyopatikana katika mwaka wa fedha 2017/18.

Imetolewa na
Ofisi ya uhusiano wa Jamii